AfCHPR
Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Wavuti: www.african-court.org
Simu : +255-272-510-510

MUHTASARI WA HUKUMU

BABAROU BOCOUM

DHIDI YA

JAMHURI YA MALI

MAOMBI NA. 023/2020

UAMUZI KUHUSU UKUBALIFU

TAREHE 13 NOVEMBA 2026

UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU

Arusha, tarehe 13 Novemba 2026: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) imetoa hukumu katika kesi ya *Babarou Bocoum dhidi ya Jamhuri ya Mali*.

Tarehe 16 Juni 2020, Bw. Babarou BOCOUM (Mleta Maombi) aliwasilisha Maombi kwenye Mahakama dhidi ya Jamhuri ya Mali akidai kufanyiwa ukiukaji wa haki yake ya usawa mbele ya sheria na ulinzi sawa chini ya sheria, kama inavyolindwa na Kifungu cha 3 cha Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba), Kifungu cha 10(3) cha Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala (ACDEG), Kifungu cha 3 cha Itifaki A/SP1/12/01 kuhusu Demokrasia na Utawala Bora ya ECOWAS (Itifaki ya ECOWAS kuhusu Demokrasia) na Kifungu cha 1 cha Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR); haki ya kushiriki kwa uhuru katika serikali ya nchi yake, inayolindwa na Kifungu cha 13(1) cha Mkataba; wajibu wa kuanzisha utaratibu huru, usio na upendeleo na wa kuaminika wa utatuzi wa migogoro ya uchaguzi, unaolindwa na Kifungu cha 17 cha ACDEG na Vifungu vya 3 na 7 vya Itifaki

ya ECOWAS kuhusu Demokrasia; wajibu wa kuanzisha chombo huru na kisicho na upendeleo cha uchaguzi unaolindwa na Kifungu cha 17 cha ACDEG na Vifungu vya 3 na 6 vya Itifaki ya ECOWAS kuhusu Demokrasia; na wajibu wa kuandaa uchaguzi katika tarehe au ndani ya muda uliowekwa katika Katiba na Sheria ya Uchaguzi, kwa mujibu wa Kifungu cha 2(2) cha Itifaki ya ECOWAS kuhusu Demokrasia.

Mleta Maombi aliiomba Mahakama: ibatilishe uchaguzi wa bunge ulioandaliwa kwa mujibu wa Amri Na. 2020-0010/PRM ya tarehe 22 Januari 2020 inayokutanisha bodi ya uchaguzi na kuweka tarehe za kuanza na kumalizika kwa kampeni ya uchaguzi wa tarehe 29 Machi 2020, pamoja na Hukumu ya Mahakama ya Kikatiba Na. 2020-04/CC-EL ya tarehe 30 Aprili 2020 inayothibitisha matokeo ya mwisho ya duru ya kwanza na ya pili ya uchaguzi wa bunge; iamuru daftari la wapiga kura lisasishwe, kwa mujibu wa masharti yanayotumika ya sheria ya ndani, ili kuhakikisha ushiriki madhubuti wa raia wa Mali katika utekelezaji wa haki ya kupiga kura kwa wote, pamoja na kukamilisha hatua zote zinazofuata zinazohitajika kwa ajili ya kuandaa uchaguzi kwa mujibu wa matakwa ya kisheria; kuchukua hatua zinazohitajika za kikatiba na kisheria ili kurekebisha Kifungu cha 92 cha Katiba ya Mali; Sheria ya Msingi Nambari 97-010 ya tarehe 11 Februari 1997 inayohusu sheria zinazosimamia muundo na utendaji kazi wa Mahakama ya Katiba na utaratibu wa kufuata mbele yake, kama ilivyorekebishwa na Sheria Nambari 02-011 ya tarehe 5 Machi 2002; Sheria Nambari 2016-048 ya tarehe 17 Oktoba 2016, kama ilivyorekebishwa na Sheria Nambari 2018-014 ya tarehe 23 Aprili 2018 kuhusu sheria ya uchaguzi; pamoja na Kanuni za Utaratibu wa Mahakama ya Katiba ya tarehe 28 Agosti 2002, ili kuhakikisha kuwa zinazingatia majukumu ya mkataba yanayohusiana na uanzishaji wa utaratibu wa kuaminika wa utatuzi wa migogoro ya uchaguzi, kama ilivyoelezwa na ACDEG (Kifungu cha 17), Itifaki ya ECOWAS A/SP1/12/01 (Vifungu vya 3 na 7), pamoja na dhamana zinazohusiana na kanuni ya usawa mbele ya sheria na ulinzi sawa chini ya sheria, zilizowekwa hasa katika Mkataba (Kifungu cha 3), Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (Kifungu cha 1) na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (Kifungu cha 26); kurekebisha Sheria ya Uchaguzi Na. 06-044 ya tarehe 4 Septemba

2006, kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 2011-085 ya tarehe 30 Desemba 2011 na Na. 2016-017 ya tarehe 21 Mei 2016, ili kuhakikisha inazingatia wajibu uliowekwa na Itifaki ya ECOWAS A/SP1/12/01 (Kifungu cha 3 na 6) na ACDEG (Kifungu cha 17(1)), hasa kupitia uundaji wa tume huru ya kitaifa ya uchaguzi, kwa mujibu wa viwango vya kisheria vya kimataifa kuhusu utawala wa kidemokrasia na uadilifu wa uchaguzi; na kumlipa Mleta Maombi kiasi cha faranga 100,000,000 za CFA kama fidia kwa madhara yote aliyopata, hasa madhara ya kifedha, ya kimwili na yasiyo ya kifedha, na kuamuru Serikali ilipe gharama zote.

Kwa upande wake, Mjibu Maombi aliiomba Mahakama itangaze kwamba Maombi hayo hayakubaliki.

Hakuna pingamizi lililowasilishwa dhidi ya mamlaka ya Mahakama. Hata hivyo, Mahakama iliridhika kwamba matakwa yote yalikuwa yametimizwa kuhusiana na vipengele vyote vya mamlaka yake ya kisheria. Kwa kuzingatia jambo hili, iliangalia kwa mfuatano mamlaka yake halisi, binafsi, ya muda na ya kieneo na ikabaini kwamba matakwa yote yalikuwa yametimizwa. Kwa hivyo, Mahakama ilichukua mamlaka ya kisheria ya kusikiliza Maombi hayo.

Mjibu Maombi hakutoa pingamizi lolote dhidi ya ukubalifu wa Maombi. Hata hivyo, Mahakama iliridhika kwamba matakwa yote ya ukubalifu chini ya Kanuni ya 50(1) ya Kanuni zake yalikuwa yametimizwa.

Kwa upande wake, Mleta Maombi alidai kwamba kushindwa kwa Mjibu Maombi kurekebisha daftari la wapiga kura kulisababisha jina lake liondolewe kwenye daftari hilo na hivyo kumnyima haki yake ya kupiga kura katika uchaguzi wa bunge wa tarehe 29 Machi 2020. Alidai kwamba hakukuwa na suluhu ya ndani aliyoweza kuitumia ili kupinga amri ya kuunda baraza la uchaguzi, kwani kilikuwa ni kitendo cha serikali ambacho hakiwezi kupitiwa na mahakama na kwa kuwa hakikumwathiri yeye binafsi au kupata madhara ya moja kwa moja. Aliongeza kusema kwamba maamuzi ya

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Wavuti: www.african-court.org
Simu : +255-272-510-510

Mahakama ya Kikatiba yanayothibitisha matokeo ya mwisho ya uchaguzi hayawezi kupingwa kwenye mahakama yoyote ya ndani.

Mahakama ilibaini kwamba sheria ya uchaguzi ya Mali inampa Mleta Maombi taratibu za ndani zinazopatikana, zenye ufanisi na za kuridhisha za kiutawala na kisheria za kupinga kuondolewa kwake kwenye daftari la wapiga kura.

Kwa kuwa haikupata ushahidi wowote katika kumbukumbu unaoonyesha kwamba Mleta Maombi alitumia taratibu hizo zilizotajwa, Mahakama ilihitimisha kwamba taratibu za ndani hazikuwa zimekamilika. Kwa hivyo, Mahakama ilitangaza kwamba Maombi hayo hayakubaliki.

Mahakama iliamua kwamba kila upande unapaswa kubeba gharama zake.

Maelezo zaidi

Taarifa zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na maelezo kamili ya hukumu ya Mahakama ya Afrika, inapatikana kwenye tovuti https://ajudata.african-court.org/details-case/0232020

Ikiwa una maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe kupitia registrar@african-court.org.

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi za Afrika ili kuhakikisha ulinzi wa haki za binadamu na watu barani Afrika. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kusikiliza kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.